

Aprili 5, 2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Tunatumai wewe na mtoto wako mko tayari kufungua shule hata kama hiyo “shule” sio jumba lililo na mkahawa na makabati lakini iko yumbani kwako. Maagizo Yasiyo ya Kiasili (NTI) yanaanza Jumanne kwa wanafunzi wote wa JCPS. Haya ni mafunzo ambayo yanayohitajika ambayo watoto watafanyia nyumbani. Walimu na wasimamizi wamekuwa wakiendesha mikutano ya mtandaoni, kupanga mipango ya mafunzo na kufahamiana na wavuti ya NTI pamoja na nakala zilishochapishwa za kazi ya shule. Tunapozindua NTI wiki hii, haya ni baadhi ya mambo unayostahili kufahamu:

- Walimu watakuwa wakifikia wanafunzi wiki hii, kueleza watachokuwa wakihitaji kutoka kwao katika NTI. Ikiwa mtoto wako hajawasiliana na mwalimu au mtu katika shule yao mwishoni mwa wiki, tafadhali wasiliana na shule au mwalimu. Unapopigia shule unaweza kusikia kurekodi kwa masaa ya baada ya shule kwenye barua ya sauti. Wacha ujumbe tu na mtu kutoka shule atakupigia simu.
- Kwa wale ambao wakp na kompyuta nyumbani, hii hapa ndio wavuti ya JCPS' NTI: <https://sites.google.com/jefferson.kyschools.us/jcps-nti/home>. Kuna ujumbe mwingi katika ukurasa hii kuhusu kuzunguka ukurasa wa wavuti na kusaidia mtoto wako. Kutoka ukurasa huu, bonyeza kwenye [Mafunzo ya NTI Yanayohitajika](#) ili kufikia kazi ya shule haswa ya shule ya mtoto wako na darasa. Kazi hii inaweza patikana kwenye kiungo cha [Tovuti za Shule ya NTI](#).
- Nakala zilizochapishwa za Choice Boards bado zinapatikana hii wiki katika zaidi ya Viwanda 60 za Chakula cha Dharura katika Louisville. Haya ni mazoezi ya elimu ambayo wanafunzi wanaweza fanyia nyumbani. Kuanza Arili 13, pakiti zilizo na nakala zilizochapishwa za kiwango cha daraja cha mafunzo zitapatikana katika viwanda vya chakula. Walimu watawasiliana na wanafunzi kuhusu kufanya kazi na nakala zilizochapishwa au mtandaoni. [Viwanda](#) vya chakula vitafunguliwa Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kutoka 10 asubuhi – 1 mchana.
- Wakati wa familia katika mpango wa Chakula cha Mchana cha Bure au Kilichopunguzwa Bei au mpango wa Elimu ya Kipekee ya Mtoto (ECE) umeisha. Barua pepe zimetumwa kwa familia ambazo zimedhibitishwa kupokea Chromebook na kutumwa kwa kompyuta kumeanzia.
- JCPS inapanga kusambaza vidude 6000 vya Wi-Fi kwa familia za ECE ambao hawana ufikiaji wa mtandao kwa sasa. Hii itawezesha watoto walio na mahitaji ya kipekee kuendelea na matibabu yao na kupokea maagizo ya kibinafsi kupitia mtandao. Familia hizi zitakuwa zinapokea maagizo juu ya jinsi ya huitisha kidude
- Wafanyikazi katika shule zetu nyingi wamekuwa wakifanya vielezo vya magari katika mitaani na kutafuta njia za kipekee za kuonyesha wanafunzi na familia jinsi tunawakosa. Hii hapa ni video ya raha kutoka wafanyikazi wa Barret Middle School ambayo ni mfano ya wafanyikazi ya JCPS wakijaribu kujihusisha na wanafunzi katika wakati huu mgumu: <https://youtu.be/Qt-ikKea4VQ>.
- Tunataka kushiriki video na picha za wanafunzi wetu pia. Tumia alama ya reli #WeAreJCPSAtHome na @JCPSKY ikiwa unatuma kitu kwenye mitandao ya kijamii.

Tunafahamu walimu, wasimamizi, familia na wanafunzi watakumbana na changamoto tunapotumia NTI kwa wanafunzi karibu 100,000. Wilaya zingine kubwa za shule za mijini zimehitimisha kuwa ni ngumu sana. Lakini tunaamimi ni jambo la busara la kufanya-kujitahidi ili kuwezesha watoto wetu kuendelea na kusoma-katiwa wakati usio wa wakawaida katika historia.